Nº250

DAWASA YETU

WIKI HII - TOLEO NA: 250 TAREHE: 10.11.2026 - 19.11.2026

MADIWANI KINONDONI WAUNGA MKONO MIPANGO YA UDHIBITI UPOTEVU WA MAJI



Madiwani Wilaya ya Kinondoni wameahidi kushirikiana na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (**DAWASA**) kudhibiti upotevu wa maji unaosababishwa na wizi na mivujo ya mabomba, hatua inayolenga kuongeza upatikanaji wa huduma kwa wananchi.

Madiwani hao kutoka Kata zote **20** wametoa ahadi hiyo katika kikao kazi na **DAWASA** kilicholenga kujenga uelewa kuhusu usimamizi wa huduma za maji, utekelezaji wa miradi na nafasi ya viongozi wa maeneo katika kulinda miundombinu na kudhibiti upotevu wa maji.

Akifungua kikao hicho, Mwakilishi wa Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Warda Abdallah, ameishukuru **DAWASA** kwa kuwapa madiwani fursa ya kutembelea miradi, vyanzo vya maji na **Mtambo wa Uzalishaji Maji wa Ruvu Chini** ili kujionea na kujifunza kuhusu jitihada za kuboresha huduma.

"Niwapongeze **DAWASA** kwa jitihada za kuboresha huduma ya maji katika Wilaya ya Kinondoni. Ni muhimu kuendeleza ushirikiano katika kudhibiti upotevu wa maji unaosababishwa na mivujo na wizi wa maji ili huduma iendelee kuimarika na kuwafikia wananchi wengi zaidi," amesema Warda.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi **DAWASA**, **Mhandisi Romanus Mwangingo**, amesema upotevu wa maji ni changamoto kubwa kwa mamlaka hiyo na kwamba mafanikio ya kuidhibiti yanategemea pia ushirikiano wa viongozi wa maeneo na wananchi.

Amesema **Waheshimiwa Madiwani na watendaji wa kata** wana nafasi muhimu ya kuhamasisha jamii kulinda miundombinu ya maji na kutoa taarifa kuhusu vitendo vya wizi pamoja na mabomba yanayovuja.

Akichangia katika kikao hicho, Diwani wa Kata ya Magomeni, **Mhe. Nordin Hassan** amesema wizi wa maji bado ni changamoto katika eneo hilo, licha ya baadhi ya wahusika kukamatwa na kutozwa faini. Ameeleza kuwa baadhi yao wamekuwa wakirejea katika vitendo hivyo baada ya kuchukuliwa hatua.